102/3 KISWAHILI (2017)

KARATASI 3 (*Fasihi*) ***Mwongozo Wa Kusahihisha***

1. a) Kuonyesha jinsi mwanasiasa fulani alivyojipendekeza kwao wakampa kura kisha baadaye akawageuka na kutowajali.

b) Msuko – kibwagizo kifupi.
- Ukaraguni – vina vya nje vinatiririka vya undani vinabadilika badilika
- Tarbia – mishororo mine
- Mathnawi – vipande viwili
- Kikwamba – neno siwe kuanzia kila ubeti *(alama 3)*
-

c) Inkisari – mfano: Siwe – si wewe
Ulosema – uliyesema – apate ulinganifu wa mizani
Lahaja – mfano; Mato – Macho
Kuboronga sarufi – Mfano: Vyaja kutoka vitisho – vitisho vyaja kumtoka
Tukujua yetu shari – tukujua shari yetu – apate urari wa vina ***(alama 3)***

d) Maswali ya balagha – maswali chochezi yasiyo na majibu
Mfano:
Bungeni tukuajiri? Kutaja – alama 1
Nawe ndiyo hiyo nari? Maelezo – alama 1
Tkupe kura waziri mfano – alama 1

e) – Alianza ulaghai
- Ukubwa ukampa kiburi
- Aliingilia raha
- Akawa aseme kuwa watu wanamharibia muda
- Akawaacha na kujiunga na matajiri wenzake
- Akazidisha tama
- Ana masidisi na anawadharau wenzio na mafari ***(alama 3)***
-

f) Si wewe uliyetuacha na kuenda bila ya kutuaga mbona usitueleze sisi ili tupate kujua makosa yetu. Hivi leo umenunua kwa hivyo kujihusisha na wasio na magari umekuwa mjeuri sana. ***(alama 4)***

g) i) Toni ya huzuni /kusikitika – anasikitika na mwanasiasa aliyewahadaa baada ya kupewa kura/ toni ya uchungu/kulalamika***(alama 2)***
ii) Mwanasiasa Fulani na wapiga kura ***(alama 1)***

©2017 Muungano Evaluators

KIDAGAA KIMEMWOZEA

2. Athari za elimu kwa wanasokomoko
   (i) Elimu inasababisha utengano na kutoelewana kati ya ndugu wawili—Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu
   (ii) Elimu inasababisha viongozi kuwanyanyasa raia, Nasaba Bora analazimisha kila mtu kuchangia karo ya kumpeleka Madhubuti ng`ambo
   (iii) Elimu inasababisha matabaka kuibuka katika jamii ya Sokomoko. Kunatokea tabaka la maskini na matajiri
   (iv) Elimu inaendeleza ufisadi katika jamii . Nasaba Bora alifika daras la nane na alipoajiriwa katika wizara ya ardhi kama karani aliendeleza ufisadi
   (v) Elimu inaendeleza wizi wa mawazo. Majisifu anauiba mswada wa Amani na kuchapisha kwa jina lake
   (vi) Elimu inaelekeza watu katika ajira .Nasaba Bora anapanga kuhongana ili Madhubuti apate kazi katika kikosi cha wanahewa.
   (vii) Elimu inasababisha uasi. Baada ya Madhubuti kupata elimu ma kurejea nyumbani, anaasi uongozi wa babake na kupigania mabadiliko.
   (viii) Elimu inatumiwa kama chombo au silaha ya kuleta mabadiliko katika jamii iliyokandamizwa na viongozi wake.
   (ix) Elimu inawabadilisha watu na kuwafanya wadanganyifu. Mwalimu Majisifu anaishi kwa kuwadanganya raia.
   (x) Elimu inawafanya watu kuwa na mapuuza .wauguzi wanapuuza matibabu ya kitoto Uhuru na baadaye kinaaga dunia
   (xi) Elimu inamdunisha na kumtenga mwanamke katika jamii. Imani anashindwa kuendelea na masomo yake kwa kukosa karo, Lowela na Mashaka hawaonekani kukamilisha masomo yao.
   (xii) Elimu inapalilia umoja na ushirikiano miongoni mwa vijana. Amani na Madhubuti wanashirikiana kwa sababu ya elimu waliyonayo, wanashirikiana kumwonelea Nasaba Bora kutoka uongozini.
   (xiii) Elimu inasababisha uozo wa maadili katika jamii. Nasaba bora ana uhusiano wa kimapenzi na Lowela Maozi,mwanafunzi wa kidato cha tatu
   (xiv) Elimu huwafanya walioelimika kuwa watalii/kutalii nchi za kigeni mfano Fao, Madhubuti, Majisifu.

3. (a) Mawazo ya mwandishi kumhusu Amani , alikuwa amelazwa kitandani katika hospitali ya Nasaba Bora baada ya kupigwa na Mtemi alipopatikana katika chumba chake cha kulala.alikuwa ametembelewa na Imani.
   (b) Alikuwa amejeruhiwa kutokana na pigo katili la Mtemi Nasaba Bora alipompata akiwa na Zuhura katika chumba chake cha kulala na kumshuku Amani kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Zuhura.
   (c) Alipigwa na tajiri wake nusura auawe baada ya kupatikana chumbani mwa tajiri wake akimsaidia mkewe kutafuta panya.
   (d) (i) Alimzuia Imani kujitosa majini .
   (ii) Alikubali Imani waandamane naye katika safari ndefu ya kujisaka
   (iii) Anamsaidia Dj na shati lake baada ya kaptula yake kutafunwa na fahali.
   (iv) Alifanya kazi nyingi kwa Mtemi bila kulalamika
   (v) Anajitolea kukilea kitoto Uhuru ambacho hakikuwa chake
   (vi) Alimsaidia Zuhura kumtunza Mashaka alipokuwa amepagawa
   (vii) Alimsaidia Zuhura kumtafuta panya aliyekuwa akimsumbua chumbani
   (viii) Aliwaomba kina Oscar Kambona kutomwua Mtemi alipowakuta barabarani wakiwa wamemzuia akiwa na Lowela.
   (ix) Alimsamehe Mwalimu Majisifu kutokana na wizi wa mswada wake
   (x) Alikubali kushirikiana na Madhubuti ili kuleta mabadiliko katika jamii
   (xi) Alimsamehe Mtemi Nasaba Bora mwishowe
   (xii) Anawatuza wale walioteswa na kufukarishwa na uongozi katili wa Mtemi Nasaba Bora
   (xiii) Alikataa kumwua Mtemi alipompa bunduki ili aitumie kumwua
   (xiv) Alikishughulikia kitoto Uhuru kilipokuwa kigonjwa

MSTAHIKI MEYA

4. (a)
   - Maneno haya yanasemwa na Gedi.
   - Alikuwa akimwambia Meya akiwa an Diwani I na II ofisini mwa Meya.
   - Hii ni kuhusiana na kutowezekana kwa ndege kutua
   - kwenye uwanja wa ndege wa Cheneo.kutokana na ukosefu wa maji safi na kugoma kwa wafanyikazi wa uwanja wa ndege na wale wa kuuza mafuta.
   - Pia anawelezea kuhusu mhazili ambaye amegoma kwa kutowezekana kwake kufika kwa Meya kutokana na mgomo wa wafanyakazi wa kuuza mafuta. *(4 x 1 = 4)*

   (b)
   - Ukosefu wa maji safi.
   - Ukosefu wa mafuta ya usafiri.
   - Kuchelewa kwa mishahara.
   - Ukosefu wa matibabu bora.
   - Ukosefu wa chakula bora.
   - Ukosefu wa vifaa k.m glovu.
   - Kutozwa kodi. *(zozote 4 x 1 = 4)*

   (c)
   - Viongozi wao hawakuwa na sera bora.
   - Mishahara ilikuwa ikicheleweshwa.
   - Mazingira walimofanyia kazi zao yalikuwa mabovu na machafu.
   - Hawangeweza kupata chakula bora na cha kushibisha.
   - Ukosefu wa matibabu katika zahanati na hospitali za Cheneo.
   - Kudharauliwa na kuteswa na watu waliolipwa pamoja na askari wa mji.
   - Ufisadi wa viongozi.
   - Elimu duni.
   - Usafiri mbaya.
   - Kubaguliwa kazini mf kutozwa kodi. *(zozote 6 x 2 = 12)*

5.
- Umaskini
- Njaa
- Utumwa
- Ufisadi
- Vitisho
- Ulaghai
- Udikteta
- Viongozi kupewa mamlaka yasiyofaa
- Ubarakala
- Kutowajibika
- Ukosefu wa haki
- Magonjwa/Ukosefu wa matibabu
- Ubadhirifu wa mali ya umma
- Ubinafsi
- Uongozi mbaya
- Kutaja 1 kufafanua 1 10×2=20

HADITHI FUPI

6.

Mke Wangu

Ndoa kati ya msimulizi na Aziza

i) Kuhitilafiana kimawazo na kimitazamo
ii) Matumizi ya lugha ya dharau upande wa Aziza
iii) Utegemezi uliozua mgogoro baina yao.
iv) Kazi –Aziza hapendenzwi na hali kuwa anafanyiwa kazi na Mapanya .
v) Mahusiano ya jamaa na marafiki kwa mfano ,msimulizi na Seluwa yanayoleta mafarakano .

Maeko

Duni na Jamila

i) Ulevi
ii) Matusi
iii) Kuchelewa kufika nyumbanmi.(Duni)
iv) Fitina kutoka kwa jamaa na marafiki mf. shangaye Jamila na Ali rafikiye Duni .
v) Mapigo

Mwana wa Darubini

Bwana Mwatela na Bi. Mwatela

i) Ulevi
ii) Uzinzi
iii) Mapingo
iv) Ubabe dume

Kanda la usufi

Mzee Butali na mkewe

i) Lawama –Mzee Butali anamlaumu mkewe pindi Sela anaporingwa na masazu.
ii) Kufurushwa –Mzee Butali anawafurusha Sela na mamake kutoka nyumbani.
iii) Ubabedume –Mzee Butali hawasikizi Sela na mamake kwa vyovyote vile.

Masazu na Sela

i) Ujmaskini
ii) Ukosefu wa Ajira /ajira hafifu
iii) Utegemezi –Mtoto wao analelewa na wazazi wake Sela.

Ndoa ya samani

Mzee kadiri na mkewe

i) Tamaa ya mali
ii) Kushindana kimajukumu
iii) Nyemeleo la ndugu na marafiki
iv) Mapuuza –kupuuza kwa mila na desturi. 4x5=20

FASIHI SIMULIZI

7. a) Misimu

Misimu ni semi za muda mbazo hubuniwa katika mazingira maalum katika kipindi maalumu cha wakati. Misimu pia huitwa simo, Misimu inaweza kupata mashiko katika jamii na kukubaliwa kama msamiati au semi rasmi za lugha. ***(alama 2)***

b) Sifa za misimu

- ✓ Misimu ni semi au msamiati ambao huzuka na kutoweka baada ya muda Fulani.
- ✓ Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi Fulani cha wakati na mahali Fulani.
- ✓ Hutumiwa na kundi Fulani la watu kufanikisha mawasiliano. Kwa mfano, kuna misimu ya vijana, ya wanyikazi katika vyombo vya usafiri na hata ya watoto.
- ✓ Ingawa misimu huzuka na kutoweka baada ya muda, baadhi ya misimu hudumu na kukubalika kama semi au msamiati sanifu wa lugha husika. Kwa mfano, neno chai (kama maana ya hongo) lilianza kama msimu , kisha likashika na kukubalika kama msemi sanifu.
- ✓ Misimu hupata maana yeke kutoka kwa watumiaji pamoja na muktadha wa mahali au wakati. Kwa mfano, neno sare ni msimu uliopata maana katika sera ya usafiri wa matatu likamaanisha kubebwa bila malipo. Aidha , pauni ya uingereza ilipokuwa thamani ya shilingi ishirini za Kenya, noti ya shilingi ishirini ilirejelewa kama pauni. Baada ya mabadiliko ya wakati na kiuchumi, ilikuja kurejelewa kama mbao. Huenda neno hili litabadilika tena au liusalie hivyo.
- ✓ Misimu si semi sanifu, hivyo haipaswi kutumiwa katika miktadha rasmi.
- ✓ Misimu huundwa kwa mbinu mbalimbali kama vile kutohoa maneno au kugeuza mpangilio wake, kwa mfano risto (hadithi) kutoka neno ‘story’ la kiingereza. ***(5x2=10)***

c) Dhima ya misimu

Misimu hutumiwa kutekelea majukumu mbalimbali katika jamii, kama ifuatayo:

- ✓ Ni kitambulisho cha kundi Fulani la watu. Misimu ya mabaharia, kwa mfano, huwatambulisha na kuwatofautisha mabaharia na vikundi vingine vya wafanyakazi katika vyombo vya bahari kama vile makuli.
- ✓ Misimu huhifadhi siri za wanaotumia. Watu hutumia misimu ili kulinda siri zao zisijulikane
- ✓ Hutumiwa kuibua hisia mbalimbali miongoni mwa wazungumzaji. Kwa mfano, waasi wa misimu chunga na ndizi ncini Kenya wakati wa kura ya maoni kuhusu katiba mpya mwaka wa 2005 waliitumia misimu hii kunadia wito wao wa kupinga au kuunga mkono katiba hiyo.
- ✓ Hukuza ushirikiano, uzalendo na uaminifu miongoni mwa wanaoitumia. Lugha ni nyenzo kuu ya kuwaunganisha watu, hivyo wanajamii wanapotumia misimu sawa, hujiona kuwa na mionjo, hali na maazimio sawa.
- ✓ Huongeza haiba au ladha katika lugha, hivyo huondoa ukinaifu unaotokana na kutumia msamiati uliozoeleka miaka nenda miaka rudi.
- ✓ Hutumia kupunguza makali katika lugha au kutasfidi lugha. Badala ya kutumia neno la aibu au msamiati unaoibua masikitko, watu hubuni misimu kueleza jambo kwa njia nyepesi isiyoumiza.
- ✓ Hukuza lugha zaidi. Wakati mwingine misimu hukubalika kama msamiati rasmi, misemo, methali au nahau katika lugha Fulani. Kwa mfano, maneno matatu na daladala ni misimu iliyoibuka kurejelea magari ya uchukuzi wa umma nchini Kenya na Tanzania mtawalia. Kwa sasa, maneno haya yanakubalika kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiswahili.
- ✓ Huhifadhi utamaduni na historia ya jamii. Kwa vile misimu tofauti hutumiwa katika vipindi mbalimbali vya wakati, kuwapo kwake huakisi maendeleo, ukuaji, historia namabadiliko katika jamii husika.
- ✓ Ni kielelezo cha mpangilio (mfumo) wa jamii Fulani , jamii na kiuchumi. Kwa vile misimu hutambulisha matabaka katika jamii, tunaweza kutambua ni matabaka gani yanayounda jamii hiyo.
- ✓ Hutumiwa kuondoa urasmi katika mazungumzo. Vijana kwa mfano wanapotumia misimu badala ya semi sanifu, huondoa urasmi na kudumisha uhusiano wa kirafiki.
- ✓ Hukuza uwezo wa kufikiri na kuthamini au kudadisi. Ili kuelewa misimu Fulani, ni lazima ufikirie na kutathmini chanzo cha msamiati huo. Mathalani Mukoloni (mama) ni mfano wa msimu wa nyumbani. Ili kuelewa, inabidi ufikirie zaidi na kupima ni nani aliye na tabia za kuthibiti watoto zaidi kati ya mama na baba. ***(4x2=8)***

8. a) Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalumu cha mwaka. ***(1x2=alama2)***

b) **Sifa za miviga**

- ✓ Miviga huandamana na matendo Fulani k.m kucheza ngoma, kupioga magoti
- ✓ Huongozwa na watu mahususi k.m kuna wanaongoza kafara
- ✓ Huandamana na utoaji mawaidha/ulumbi
- ✓ Maleba huvaliwa na wanaohusika
- ✓ Hufanyiwa katika mazingira maalum
- ✓ Huambatana /hufungamna na utamaduni wa jamii husika
- ✓ Hufanya katika kipindi/wakati maalum
- ✓ Huwa na kutolewa kafara
- ✓ Sadaka hutolewa
- ✓ Kuna kula viapo – wahusika huweka ahadi kutenda wema ***(zozote 5x1=alama5)***

c) Udhaifu

- ✓ Husababisha kudorora kwa maendeleo
- ✓ Huleta utengano kati ya jamii/majirani
- ✓ Huasi mabadiliko ya kiwakati (nyingine zimepitwa na wakati)
- ✓ Madhara yaweza kutokea hasa vifaa butu vinapotumika
- ✓ Huleta utengano wa kijinsia, kumtukuza mwanaume na kudunisha mwanamke k.m jando na unyango ***(zozote 3x1=alama3)***

d) **Umuhimu wa ngomezi**

- ✓ Ni njia ya kuwasiliana katika jamii husika
- ✓ Hudumisha usiri wa jamii husika
- ✓ Hutumiwa kutangaza matangazo muhimu kuhusu shughuli maalum
- ✓ Huendeleza utamaduni wa jamii
- ✓ Huisaidia jamii kuionea fahari historia yao
- ✓ Hutahadharisha kuhusu matokeo ya dharura
- ✓ Hudhihirisha ufundi wa kisanaa (kutumia zana Fulani za muziki)
- ✓ Hutekeleza majukumu ya maandishi katika jamii zisizojua kuandika
- ✓ Huburudisha ***(zozote 6x1 = alama 6)***

e) Vizingiti

- ✓ Mwingiliano wa makabila tofauti hauruhusu tena matumizi ya ngomezi
- ✓ Maendeleo ya teknolojia hayaruhusu ngomezi k.m barua, simu
- ✓ Watu wamekuwa wabinmfsi – hawawezi kuitika ngoma ikipigwa
- ✓ Ukosefu wa usalama – watu kushambiliwa wakiitikia wito wa ngomezi ***(zozote 2x1=alama 2)***